Sheria za Unywaji Pombe na Uendeshaji Gari

Unywaji pombe husababisha mabadiliko kwenye ubongo na mwili ambayo huweza kufanya uendeshaji kuwa hatari kwa dereva. Mabadiliko ambayo huathiri uendeshaji mzuri ni: kuona na kusikia hafifu, kuamua kulikoathirika, utambulizi na ukarabati pungufu na kusinzia. Maafisa wa polisi wanaweza kutambua kiwango cha pombe ambacho mtu amekunywa kwa kupima wingi wa pombe kwenye damu yao (BAC). Nchini Marekani, ni haramu kisheria kuendesha gari ikiwa BAC yako inazidi asilimia 0.08. Majimbo mengine yana vikomo vya chini zaidi vya BAC kwa watoto na madereva wa kibiashara. Ikiwa utasimamishwa na kupatikana kuwa una BAC iliyo juu ya kikomo kinachoruhusiwa kisheria, unaweza kushtakiwa na kosa la kuendesha gari ukiwa umelewa, ambalo linajulikana pia kama DWI, DUI, au uendeshaji gari ukiwa umelewa.

Je ni vinywaji ngapi vinavyokufikisha kwenye kikomo halali? Hakuna jibu moja sahihi kwa swali hili. Kuna vikokotozi na chati ambazo zinaweza kukadiri wingi wa pombe kwenye damu yako kulingana na kiasi ambacho umekunywa. Hata hivyo, chati hizi zinapaswa kutumika kama rejeo tu. Kila mtu ana sifa za kipekee za kimwili kama uzani, jinsia, asilimia ya mafuta yaliyo mwilini na maumbile ambazo huchangia pakubwa katika kuamua kiwango chao cha BAC.

Je ni nini huchangia kinywaji kimoja? Nchini Marekani, kinywaji kimoja cha wastani ni kinywaji chochote kilicho na takriban ounce 0.6 za ugiligili au gramu 14 za pombe "tupu". Ijapokuwa vinywaji vilivyo kwenye picha hapa chini ni vya saizi tofauti, kila moja yavyo kina takriban kiasi sawa cha pombe na kinachangia kinywaji kimoja.

Picha kutoka:
http://pubs.niaaa.nih.gov/publications/RethinkingDrinking/Rethinking_Drinking.pdf

Swahili Translation Date: February 2016

Uamuzi salama zaidi ni 'usinywe ukaendesha gari'. Kuna sheria kali sana za uendeshaji gari ukiwa umelewa. Ukinywa kisha uendeshe gari, unahatarisha uhuru wako, fedha zako na siku zako za usoni.

Maelezo yafuatayo yanatoa mwongozo kuhusu adhabu na vikwazo/marufuku unayoweza kuyatumikia iwapo umeshikwa kwa kuendesha gari ukiwa umeathirika. Kuna sheria zaidi, adhabu na vikwazo/marufuku kwa walio chini ya miaka 21, unapokuwa na BAC ya juu zaidi, na ikiwa kuna mtoto garini mwako. Miongozo hii inahusu makosa yanayotendeka katika kipindi cha ndani ya miaka 10.

Mara ya 1 ambayo mtu anafungwa kwa uendeshaji gari akiwa amelewa, leseni yao ya uendeshaji inaweza kusimamishwa (kuchukuliwa) kwa muda fulani. Dereva yule pia atalazimika kulipa faini na/au atumikie kifungo gerezani. **Kila wakati ambapo** dereva anapoteza leseni yake kwa sababu ya DWI, huwa anahitajika kutimiza matakwa fulani ili arudishiwe leseni yao ya uendeshaji, kama kulipa faini ya ziada, na kukamilisha jaribio la ujuzi wa DWI, kuomba leseni ya uendeshaji, na kuchunguziwa uwepo wa kemikali.

Mara ya 2 ambayo mtu anafungwa kwa uendeshaji gari akiwa amelewa, leseni yake ya uendeshaji gari husimamishwa kwa angalau muda mrefu zaidi. Pia huwa analipa faini kubwa zaidi na/au kutumikia kifungo cha muda mrefu zaidi gerezani. Nambari zao za usajili za gari huenda zizuiliwe, inayomaanisha kuwa zitachukuliwa na kubadillishwa na nambari maalumu ya usajili ambayo hutolewa tu kwa walioshtakiwa na DWI. Pia huwa anahitajika kutimiza matakwa fulani ili arudishiwe leseni yake ya uendeshaji.

Mara ya 3 ambayo mtu ameshikwa kwa sababu ya DWI, yeye hupoteza leseni yake ya uendeshaji kwa muda mrefu zaidi na huhitajika kulipa faini kubwa zaidi na/au kutumikia kifungo kirefu zaidi gerezani. Nambari zao za usajili za gari zinaweza kuzuiliwa, na gari lao kuchukuliwa kabisa inayomaanisha kuwa polisi watalichukua milele na mwenye gari hatawahi lipata wala hatalipwa chochote. Pia, dereva huyo atahitajika kutimiza matakwa fulani ili arudishiwe leseni yake ya uendeshaji. Baada ya DWI 3, dereva huyo huenda akahitajika kuzuru kituo cha matibabu na mageuzi na awasilishe vipimo vya kila wakati vya mkojo, ambavyo katika majimbo mengine hufanywa kwa muda wa mwaka mmoja, kuthibitisha kwamba hanywi pombe.

Mara ya 4 ambayo mtu ameshtakiwa kwa DWI ndani ya miaka 10, huenda ashtakiwe na kosa la uhalifu mkali. Leseni yake ya uendeshaji huenda ibatilishwe kwa muda wa miaka 4 na aamriwe azuru kituo cha matibabu na mageuzi na awasilishe thibitisho la kuacha unywaji pombe kwa muda wa angalau mwaka 1. Uachaji pombe kabisa kabisa maishani huenda uhitajike baada ya urejesho. Kwa mfano, katika Minnesota mnamo 2015, waliofungwa kwa uhalifu mkali wa DWI waliweza kutumikia kifungo cha miaka 7 gerezani na kuweza kuachiliwa na masharti baada ya miaka 5 pamoja na faini ya $14,000.

Kosa la DWI linaweza kuathiri hali yako ya uhamiaji. Mtu anaposhikwa kwa DWI, polisi huchukua alama zao za vidole na picha zao na kuweka maelezo yao kwenye hifadhidata ya kitaifa. Mtu huyo atakuwa na rekodi ya uhalifu ya kudumu. Kuwa na

rekodi ya uhalifu kunaweza kumwathiri mtu vibaya hasa anapoandika ombi la kubadilisha hali yake ya uhamiaji. Kwa mfano, inaweza kusababisha unyimwe Green card au uraia, au, katika hali zingine mbaya zaidi, inaweza kukusababishia kufukuzwa nchini Marekani.

ASILI: http://www.dmv.org/mn-minnesota/automotive-law/dui.php